**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**TATHMINI YA MIAKA MITANO (5) YA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA MAGEUZI WA MIAKA 10 YA SEKATA YA KARAFUU (2011/2021)**

Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) lilijiwekea Mkakati maalum wa miaka 10 (2011 -2021) wa Mageuzi katika Sekta ya Karafuu ambapo sasa tumefikisha miaka mitano ya utekelezaji wa Mageuzi hayo. Lengo kuu la Mkakati huu ni kurudisha hadhi na thamani ya zao la Karafuu kwa maendeleo ya Zanzibar.

Yalikuwa maelekezo ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein ambapo aliangalia zaidi mabadiliko ya kimaisha na mtazamo wenye kuleta tija na maendeleo ya nchi kwa kuipa hadhi na msukumo wa kipekee Sekta ya Karafuu.

Mkakati huu wa Mageuzi katika Sekta ya Karafuu unakwenda sambamba na Mkakati wa kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini, Zanzibar (MKUZA II) na Changamoto za Milenia" kwa vile kuimarika kwa Sekta ya Karafuu ni kuimarika kwa uchumi wa nchi, kuongezeka kwa ajira, kuimarika kwa kipato cha Wakulima na Wananchi wanaotegemea zao hili na kupungua kwa umasikini.

Katika miaka hii ya mwanzo (2011 -2016), hatua maalum zimechukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuongeza uzalishaji, usafirishaji, ubora na tija kwa Wakulima na Serikali kwa ujumla.

Serikali imefanya Mageuzi makubwa katika Sekta nzima ya Karafuu ikiwa ni pamoja na kutengeneza Sheria, Sera na Miongozo madhubuti ya kusimamia Sekta hii ambapo faida, tija na ustawi wa maisha ya wanaotegemea kupata kipato katika zao hili unaonekana.

Tafiti mbalimbali zilifanywa na Serikali kwa kutumia Wataalamu iliyowapa kazi ya kufanya Utafiti juu ya namna ya kufanya Mageuzi katika Sekta hii. Hatimae mapendekezo yalitolewa na kufanyiwa kazi

kwa kutatuliwa kwa matatizo na kuzikabili changamoto zilizokwaza Maendeleo ya Sekta ya Karafuu.

**Bei ya kununulia Karafuu kutoka kwa Mkulima:**

Serikali ya Awamu ya Saba chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Shein alitoa kipaumbele zaidi maslahi ya Wakulima katika Mageuzi ya Sekta hii kwa kuanza kubadilisha Sera ya Malipo kwa Wakulima kwa lengo la kuwanufaisha zaidi.

Serikali ilitangaza bei ya kununulia karafuu kutoka kwa Mkulima kuwa asilimia 80 ya bei ya kuuzia karafuu nje. Bei hii imewatia ari na moyo Wakulima kuliimarisha zaidi zao hili kwa kupanda Mikarafuu mingi zaidi, kuihudumia mashamba na kuuza karafuu zao Serikalini.

Katika miaka mitano hii ya utekelezaji wa Mageuzi, Wakulima wameuza karafuu zao kwa ZSTC kwa wastani wa bei ya TZS 14, 000 kwa kilo badala ya TZS 5, 000 bei iliyokuwepo mwaka 2010. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 180.

**Kutungwa kwa Sheria:**

Mnamo mwezi Disemba, 2011, Dkt. Shein alitia saini Sheria mpya ya ZSTC Na. 11 ya mwaka 2011 inayolipa mamlaka na uwezo Shirika la ZSTC kulisimamia, kulihudumia, na kuliimarisha zao la Karafuu na kuhakikisha linakuwa endelevu kwa maslahi ya Wakulima, Wananchi na Taifa kwa ujumla. Kupitia Sheria hii, Shirika la ZSTC lilifanyiwa marekebisho katika Muundo wake wa Uongozi na Uendeshaji, Sheria hii imeliwezesha Shirika kufanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa.

Serikali ya Awamu ya Saba pia ilipitisha Sheria mpya ya maendeleo ya Karafuu Na. 2 Mwaka 2014 pamoja na Kanuni zake kwenye mwaka huo huo wa 2014.

Kupitia Sheria hii ya Maendeleo ya Karafuu, chini ya kifungu Na. 4 (1), Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu umeanzishwa. Katika kipindi cha miaka mitano Mfuko huu ambao upo chini ya Shirka la ZSTC umetekeleza vyema na kwa ufanisi kazi za kuimarisha, kuindeleza na kusimamia Sekta ya Zao la Karafuu Zanzibar.

## Kuimarika kwa Uzalishaji na Usafirshaji wa Karafuu:

### *Manunuzi*

Utekelezaji wa mkakati huu umeleta mafanikio makubwa kwa Sekta hii kwani kwa kipindi cha miaka mitano (2011/12 – 2015/16) jumla ya tani 20,323.00 za karafuu zenye thamani ya TZS 286.86 bilioni zimenunuliwa kutoka kwa Wakulima. Kwa maana hiyo, katika kipindi cha miaka hiyo mitano, Wakulima wa Karafuu wamejipatia jumla ya TZS 286.86 bilioni kutoka TZS 42.6 bilioni miaka mitano kabla ya utekelezaji wa mkakati huu wa Mageuzi, Ongezeko hili la fedha zilizoingia mifukoni mwa Wakulima ni asilimia 80.

### *Usafirishaji*

Usafirishaji wa karafuu nje ya nchi umeongezeka kutoka tani 13, 004. 46 zenye thamani ya US $45.29 milioni zilizouzwa nje ya nchi kwa kipindi cha 2005/06 – 2009/10 na kufikia tani 20, 142.17 zenye thamani ya US $212.24 milioni zilizouzwa katika kipindi cha miaka mitano (2011 /12 – 2015/16).

## Uimarishaji wa Ubora wa Karafuu:

Pamoja na kutoa elimu kwa Wakulima juu ya namna ya kulinda ubora wa zao la karafuu, Shirika limenunua mashine tano (5) maalum za kusafisha karafuu kabla ya kusafirishwa nje ya nchi kwa mauzo, lengo ni kuhakikisha kuwa karafuu zinazosafirishwa kwa mauzo zinakuwa safi.

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Shirika limempa kazi Mkemia Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufanya Utafiti juu ya sifa halisi za karafuu ya Zanzibar (Vinasaba) kwa ajili ya kuzifanyia Utambulisho maalum (BRANDING), kukamilika kwa mpango huu kutaungeza thamani na tija ya zao hili kwa Wakulima na Serikali.

## Elimu kwa Wakulima:

Katika kipindi cha miaka mitano, suala la elimu kwa wakulima wa zao la karafuu limezingatiwa na kupewa umuhimu mkubwa. Elimu imetolewa kupitia njia zote za Mawasiliano kama vile; Vyombo vya Habari, Mikutano ya Wakulima na Wadau wengine wa zao la Karafuu, Maonesho ya sinema Vijijini pamoja na Machapisho mbalimbali likiwemo Jarida Maalum (Zanzibar Cloves Magazine), ambalo huchapishwa mara mbili kwa mwaka.

Elimu hiyo ilihusu zaidi uadilifu katika kufanya biashara ya karafuu, tathmini ya utekelezaji wa kazi za vuno kwa kipindi husika, kuzingatia ubora na usafi wa karafuu ili kulinda hadhi na sifa za karafuu za Zanzibar. Aidha, elimu katika upandaji, uhudumiaji na uimarishaji wa Mikarafuu kwa lengo la kuongeza idadi ya Mikarafuu pamoja na wingi wa uzalishaji wa zao hili imetolewa.

## Huduma kwa Wakulima

Mpango wa Serikali ya Awamu ya Saba wa kuliunda upya Shirika la ZSTC kwa Sheria mpya Na. 11 ya mwaka 2011 kumeliwezesha Shirika kwa kiasi kikubwa kutoa huduma kwa Wakulima na kujiendesha kwa ufanisi.

### *Mikopo kwa Wakulima*

Shirika limeweza kuwahudumia Wakulima kwa kuwapa mikopo isiyo na riba. Jumlaya TZS 972.7 milioni zimekopeshwa kwa Wakulima

Unguja na Pemba ambapo hutakiwa kurejesha fedha hizo bila ya ziada (riba), lengo ni kuwawezesha kujiandaa katika uchumaji za zao hili muhimu kwa uchumi wa Zanzibar.

***Fidia kwa Wakulima***

Kukiwa na utaratibu madhubuti wa kuondosha udanganyifu, Shirika limerudisha mpango wa kutoa fidia kwa Wakulima wanaopata ajali wakati wa uchumaji ili kujenga ari na moyo kwa Wananchi kushirika katika kazi za uchumaji karafuu. Shirika kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu tumetoa fidia ya TZS 186.56 milioni kwa Wakulima Unguja na Pemba.

***Misaada kwa Wakulima***

Pia, katika kipindi cha miaka mitano (5) ya Utekelezaji wa Mageuzi, Shirika limetoa vifaa vyenye thamani ya TZS 902.2 milioni kwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na kwa Vitalu vya watu binafsi kwa ajili ya kuotesha miche ya mikarafuu. Kutokana na jitihada hizo, wastani wa miche ya mikarafuu laki tatu (300, 000) hadi laki tano (500, 000) huzalishwa na kupatiwa Wakulima kila mwaka bila ya malipo.

***Ujenzi na Uimarishaji wa Vituo vya ununu wa Krafuu***

Shirika limeimarisha na kujenga Vituo vipya 22 kati ya Vituo 35 vya ununuzi wa karafuu. Vituo hivi ni vya kisasas na vipo karibu na maeneo ya Wakulima, lengo ni kuwarahisisishia usafirishaji wa karafuu kwenda katika vituo hivyo. Shirika pia linaendelea na ujenzi wa vituo vilivyobaki ili kuendana na mahitaji halisi.

***Huduma za Kijamii***

Sambamba na ujenzi wa vituo hivyo, huduma za kijamii katika Vituo hivyo kama vile maji, vyoo, umeme na sehemu za kukaa Wakulima

wakisubiri kuhudumiwa zimezingatiwa, jambo ambalo halikuwepo kabla. Adha, Vituo hivyo pia hutumika kwa shughuli za kijamii bila ya kutozwa ada yoyote.

***Kufanyiwa kazi Hoja za Wakulima***

Hoja nyingi za msingi kutoka kwa Wakulima kwenda Serikalini zikiwemo bei nzuri, vituo bora vya ununuzi, malipo ya fidia kwa wanaopata ajali wakati wa uchumaji wa Karafuu, upatikanaji wa mikopo ya uchumaji, pamoja na upatikanaji wa miche zimeshafanyiwa kazi.

## Changamoto

Miongoni mwa changamoto zinazolikumba Shirika ni pamoja na baadhi ya Wakulima kuwa na tabia ya kuchafua karafuu kwa makusudi kwa kuchanganya karafuu na makonyo, matende wakati mwengine kuleta karafuu zisizokauka inavyotakiwa katika vituo vya ununuzi.

Pia, baadhi ya Wakulima wamekuwa wakianika karafuu zao bila ya kuzingatia maelekezo ya kulinda ubora ambapo huanika karafuu zao barabarani, juu ya mabati na sakafuni, hii ni hatari kwani zinaweza kupoteza sifa za karafuu zetu ambazo zimezoeleka katika soko la nje.

Aida, kuna baadhi ya Wakulima huchelea na hata kutorudisha kabisa fedha za mikopo ya uchumaji wa karafuu. Pamoja na Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu kufanya kazi nzuri ya uimarishaji, uendelezaji na usimamizi wa Sekta ya Karafuu, bado Mfuko huu haujapata michango ya kutosha kutoka kwa Wadau ambao kwa mujibu wa Sheria na. 2 ya 2014 wanatakiwa kuuchangia.

Katika kipindi cha hivi karibuni, kumejitokeza matukio ya kukatwa kwa mikarafuu na kuchomwa moto Mashamba ya Mikarafuu, vitendo hivi vinawaumiza sana wakulima na kuwakatisha tamaa kwa sababu

Mkarafuu ni mti unaohitaji huduma kubwa katika ukuwaji wake pia ni chanzo cha kipato kwa Wananchi wengi.

## Mtazamo wa baadae

Mtazamo wa baadae wa Shirika ni kuendelea kutekeleza Mkakati huu wa Mageuzi ya Sekta ya Karafuu kwa kasi, ari na nguvu zaidi. Serikali itaendelea kutekeleza azma yake ya kutoa bei nzuri ya karafuu kwa Wakuima kulingana na kuimarika kwa bei katika soko la dunia.

Kwa kushirikiana na Wadau wengine, Shirika litaendelea kutoa elimu na huduma zaidi kwa Wakulima wa zao la Karafuu ikiwa pamoja na kusaidia ujenzi wa barabara katika maeneo yenye karafuu nyingi.

Shirika lina mpango wa kununua mashine za kupimia unyevu kwa kila kituo cha ununuzi Unguja na Pemba ili kuhakikisha kuwa karafuu zote zinaonunuliwa kutoka kwa Wakulima zinakauka kwa kiwango kinachotakiwa.

Kutokana na moyo na ari ya Wakulima katika upandaji na uhudumiaji wa Mashamba ya Mikarafuu, tunaamini kuwa uzalishaji na usafirishaji utaongezeka mwaka hadi mwaka.

Tunaomba mashirikiano zaidi kutoka kwa Wakulima na Wadau wote wa zao la Karafuu ili kutimiza lengo na azma ya Serikali ya kuongeza uzalishaji, usafirishaji na ubora kwa ustawi wa maisha ya Wananchi wa Zanzibar.

**‘KARAFUU NI UHAI, KARAFUU KWA MAENDELEO YA ZANZIBAR’**

**DKT. SAID SEIF MZEE**
**MKURUGENZI MWENDESHAJI**
**ZSTC- ZANZIBAR.**
**6 DISEMBA, 2016.**